

HALMASHAURI YA MJI WA KIBAHA



TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI YA UJENZI HOSPITALI YA WILAYA KATA YA PICHA YA NDEGE MTA A WA LULANZI(UJENZI WA WODI YA WATOTO) ZABUNI NAMBA LGA/011/2020-21/W/35 TAREHE 09-03-2021

HALMASHAURI YA MJI WA KIBAHA IMEPOKEA FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU KWA AJILI YA GHARAMA ZA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA NA INAKUSUDIA KUTUMIA SEHEMU YA FEDHA HUSIKA KULIPIA MALIPO HALALI CHINI YA MKATABA AMBAO UNATOLEWA KATIKA MWALIKO HUU.

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI WA KIBAHA ANAWATANGAZIA MAFUNDI UJENZI WA KIJAMII WA WILAYA YA KIBAHA MJI NA MAENEO YA KARIBU KWAMBA KUNA KAZI YA UJENZI WA WODI YA WATOTO HOSPITALI YA WILAYA ENEO LA LULANZI.

MWOMBAJI ANARUHUSIWA KUOMBA KWA KUJAZA FOMU MAALUM INAZOONYESHA AINA YA KAZI, UKUBWA WA KAZI NA GHARAMA YA JENGO (BOQ). FOMU HIZO ZINATOLEWA NA KITENGO CHA MANUNUZI HALMASHAURI YA MJI KIBAHA, **KWA ADA YA TSH 30,000** AMBAYO HAITAREJESHWA.

SIFA ZA MWOMBAJI;

- AWE AMEHITIMU ELIMU YA KUENZIA KIDATO CHA NNE

- AWE AMEPITIA MAFUNZO YA UFUNDI WA MAJENGO KUTUNUKIWA CHETI CHA KUFUZU MAFUNZO HAYO KUTOKA CHUO CHA UFUNDI KINACHOTAMBULIKA KISHERIA
- AWE NA UZOEFU WA UJENZI WA MAJENGO YA SERIKALI NA BINAFSI USIOPUNGUA MIAKA MITATU (3).
- AWE NA UWEZO WA KUSOMA RAMANI YA UJENZI NA KUITAFSIRI.
- AWE NA ANWANI YA ANAKOISHI
- OFISI YA MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI HAILAZIMIKI KUKUBALI GHARAMA YA CHINI ITAKAYOTOLEWA NA FUNDI.

NYARAKA YA ZABUNI KATIKA UHALISIA WAKE (ORIGINAL) PAMOJA NA NAKALA MOJA ZINAZOFANANA, ZILIZOJAZWA KWA USAHIHI NA KUWEKWA KWENYE BAHASHA ILIYOANDIKWA " MAOMBI NA. LGA/011/2020-2021/W/35 ZABUNI YA UJENZI WA WODI YA WATOTO HOSPITALI YA WILAYA LAZIMA ZIPELEKWE KWA OFISI YA MANUNUZI MAKAO MAKUU YA HALMASHAURI YA MJI WA KIBAHA S.L.P30112 KIBAHA MJI.


SIKU YA MWISHO YA KUWASILISHA MAOMBI NI SIKU YA JUMATATU TAREHE 15/03/2021 SAA TANO KAMILI ASUBUHI 5.00 MAOMBI YATAFUNGULIWA HADHARANI MARA TU BAADA YA MUDA WA MWISHO WA KUWASILISHA, MBELE YA WAOMBAJI KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO HALMASHAURI YA MJI WA KIBAHA NA WAOMBAJI WOTE WATAFANYIWA USAILI BAADA YA UFUNGUZI.

MAOMBI YATAKAYOCHELEWA KULETWA, MAOMBI YASIYOFUNGULIWA KATIKA TUKIO LA UFUNGUZI WA ZABUNI, HAYATAKUBALIWA KWA AJILI YA KUTATHMINIWA KWA HALI YO YOTE ILE.

WOTE MNAKARIBISHWA KUCHANGAMKIA FURSA HII.

IMETOLEWA NA

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA


JENIFA C. OMOLO
MKURUGENZI HALMASHAURI MJI
KIBAHA